


Tunabahati kubwa sana sisi wakazi wa Wilaya ya Kilwa kwa kuwa na maliasili ya thamani sana Duniani...

Mti wa Mpingo

Mti huu unatoa mojawapo ya mbao zenye thamani kubwa sana duniani. Mbali ya kutengenezea vinyago, huko Ulaya unatumika kutengeneza ala za muziki kama vile vinubi.



Katika mpango mpya wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu, jamii imepewa uwezo wa kutenga misitu ya vijiji katika maeneo yao. Rasilimali zote zilizomo katika misitu ya vijiji ni mali yao. Hii inamaanisha kuwa, kama mti wa aina yeyote katika msitu wa kijiji utavunwa, ada yake itabaki kijijini. Ushuru wa serikali kukata mpingo ni kama wastani wa shilingi 10,000/- kwa kila gogo.

Vijiji vilivyopo katika mpango wa Usimamizi Shirikishi wa misitu vitafaidika na mpango huu na wana uhuru wa kutumia mapato yatokanayo na rasilimali za misitu kama wapendavyo katika miradi mbalimbali ya maendeleo kijijini. Kijiji chako kitatumiaje pesa hizo?



Katika Wilaya nyingine, tayari wenzetu wako mbele na walishaanza kufaidi matunda yatokanayo na Misitu ya vijiji. Kwa mfano Wilaya ya Babati Mkoani Manyara, kuna vijiji ambavyo wamefaidika kwa kujenga nyumba bora za kuishi. Mifano mingine ni Wilaya ya Iringa vijijini kuna vijiji vilivyopata huduma ya maji safi ya kunywa na huduma za mawasiliano kutokana na kushiriki kikamilifu katika kuitunza misitu inayowazunguka.

Hakika tunatakiwa kujitahidi ili kuwafikia wenzetu, Kilwa bado tunao uoto mzuri kabisa wa miombo uliobakia hapa nchini. Kwa hiyo, vijiji vya hapa vina rasilimali halisi za asili ambazo zitahitaji juhudi zetu za kuitunza na kuiendeleza. Kama kijiji chako kimepimwa na kina hati miliki, rasilimali zote katika kijiji hicho ni mali ya jamii husika.

Usimamizi wa misitu ya vijiji ni muhimu pia ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa miti ya kujengea nyumba, kuni, madawa ya asili na matunda.

Kwa hiyo shiriki kikamilifu katika kulinda misitu kwa faida yako na vizazi vijavyo.



Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mradi wa Kuhifadhi Mpingo au Idara ya Maliasili Wilaya ya Kilwa, S.L.P. 49, Kilwa Masoko.



Kijarida hiki kimeandaliwa na Mradi wa Kuhifadhi Mpingo (MCP) kwa msaada wa Mpingo wa Tuzo ya Kuhifadhi Mazingira wa Shirika la Mafuta la BP.

Thamani ya Mpingo



Iko Mikononi Mwetu

